

# Pambazuko

Toleo Namba 076

Jumatatu Juni 17-23, 2024



Jicho la Tai

**'Dkt. Mwigulu Nchemba anataka nife haraka' UK. 5**



## Nyuma ya Bajeti 2024/25

- *Sehemu kubwa inakwenda kulipa madeni*
- *Kwa thamani ya dola, bajeti imeshuka zaidi*
- *Bado haitoi msukumo kwa sekta binafsi*

**NDANI:** Kurasa 12 za uchambuzi wa Bajeti



JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

## Tahariri

## Tuzienzi daima tunu za Mwalimu Nyerere

**I**FIKAPO Oktoba, kila mwaka, Tanzania huadhimisha kumbukizi ya kifo cha Baba wa Taifa letu na aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Mwalimu Nyerere alifariki dunia Oktoba 14, 1999 katika Hospitali ya Mt. Thomas iliyopo London, Uingereza alipokuwa akiendelea kupatiwa matibabu. Ilibainika kitabibu kwamba Mwalimu alipatwa ugonjwa wa saratani ya damu.

Wakati wa uhai wake, Mwalimu aliyeongoza Tanganyika na baadaye Tanzania, alipata sifa za kuwa kiongozi mwenye kujali utu, kuzingatia katiba na zaidi sana kuwa na uzalendo usiotiliwa shaka ya aina yoyote.

Mwalimu Nyerere hakupata sifa lukuki kwa kujipendekeza kwa “wakubwa” wala kuonea watu, hapana! Alijenga mizizi ya sifa zake za uongozi kwa kutenda haki, kujali misingi ya utu na kuikumbatia Katiba ya Tanzania, hata kama ilikuwa na “mashimo” mengi.

Mwalimu Nyerere katika kuitumikia nchi changa, kwa misingi hiyohiyo ya uzalendo, alichukua hatua kadhaa ambazo hazikupendeza, lakini alikuwa na sababu nzuri za kufanya hivyo.

Sababu hizo hazikuwa na mizizi ya kuonea, kupendelea kundi fulani au kujijengea wigo wa kuiba mali za umma kwa manufaa binafsi na familia zake.

Ni Mwalimu Nyerere ambaye alikataa kuona tabaka moja linanyonya tabaka jingine; iwe ni katika ajira, kufanya biashara na hata katika maisha mengine. Alitamani kuona kila mmoja akifurahia uhuru

wa nchi yetu uliopatikana kwa jasho na hata damu.

Baada ya miaka yake ya kuongoza – akiwa ameitumikia nchi kwa miaka 24, aliamua kung’atuka ili kuacha wengine waongoze naye akibaki kuwa mshauri.

Hata hivyo, isivyokuwa bahati, baada ya Mwalimu Nyerere kufariki dunia, Tanzania ikaanza kupata sifa mbaya ambazo hazikuwahi kuwepo wakati wa uongozi wa muasisi huyo.

Kutokuwepo kwake, kukaanza kushuhudiwa kuwepo kwa dalili za ukabila, kuongezeka kwa rushwa, matumizi mabaya ya madaraka na ufisadi wa kupindukia.

Uzalendo ukaonekana kuwa “bidhaa” adimu, kwani watu wengi, hasa viongozi wengi walioaminiwa na umma wakageuka kuwa walafi na wakwapuaji wakubwa wa mali za umma.

Undugunaizesheni, umimi na ukabila ukaonekana kutamalaki na kibaya zaidi ukifanywa bila kificho na hali hiyo ikakomaza majanga mengine na kuimarisha mnyororo wa wizi na ufisadi katika ofisi za umma.

Sasa basi, ni vyema Watanzania wakarejea kwenye misingi aliyoacha kiongozi huyo ili nchi yetu irudi kuwa rejea kila kunapojadiliwa amani, usawa, utu na uzalendo.

Ni vyema kumuenzi muasisi huyo na mwana wa Afrika kwa kukataa na kukemea madhila yote yanayofisha utaifa, umoja, upendo na utu wa Tanzania na watu wake.

Wakati tunakumbuka mema yake, tunamuomba Mwalimu Julius Nyerere aendelee kulala mahali panapostahili.

## MAMA NA WAJUKUU IKULU...



*Rais Samia Suluhu Hassan akisherehekea Siku ya Mtoto wa Afrika akiwa pamoja na wajukuu, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. Siku hii huadhimishwa Juni 16 ya kila mwaka. (Picha na Ikulu).*

### Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

### NUKUU



*Ni vyema na haki kwa kila mmoja wetu kukumbuka kujivua mzigo wa kiburi cha cheo au mali, na ajitwishe hisani, ubinadamu na tafakuri ya kujiweka katika viatu vya mwenzake - Abdulsamad Abdulrahim (mbobezi katika sekta ya nishati na madini Tanzania).*

## Tangazo

## Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagua, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

**Mhariri Mkuu,**  
**Oktoba, 2023**

## Changia Pambazuko liendelee

**WAJUMBE** wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukaza Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeviza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yameweka wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchocha umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

**Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263**

Ukituma mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandali: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchagua, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

**Lipa kwa Simu**

Lipa kwa kuscana

Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI

igmpesa | Tigo | Airtel | M-Pesa | Airtel | hola | 1020



## ‘Dkt. Mwigulu Nchemba anataka nife haraka’

Na Igo AI

**B**INADAMU mwanauume, mwanachama kindakindaki wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), mstaaafu wa miaka mingi na sasa akijitambulisha mara nyingi kuwa ni “sinia sitizeni”- mwenye jina la Mzee Tai, anamlaani Daktari Mwigulu Nchemba.

Anamlaani waziri huyo wa fedha wa Tanzania, kwa madai kuwa Daktari Mwigulu Nchemba, amepanga kuhakikisha kuwa anaondoka haraka juu ya uso wa dunia hii ya Mungu kwa kuwa ameamua “kumkata miguu.”

Kwamba Daktari Mwigulu Nchemba, yule Mbunge wa Iramba Magharibi, amefanya makusudi ‘kumnyang’anya’ huyo sinia sitizeni usafiri wake uliokuwa ukimsaidia kwenda huko na kule kwa urahisi zaidi.

Kwamba Daktari Mwigulu Nchemba kuutangazia umma wa Watanzania, tena akiwa ndani ya Bunge jijini Dodoma, na akisikilizwa na kutazamwa na dunia nzima kupitia televisheni, kuwa sasa ataanza kutoza kodi kwenye gesi- asilia inayotumika kwenye magari ni wivu tu kwa sinia sitizeni.

“Huyu Daktari Mwigulu Nchemba, namfahamu sana, miaka yote ameona nafaidi sana kuendesha magari kangu, yaani mimi kuachana na matumizi ya mafuta yao, anaona nafaidi sana na sasa kaamua kunikata miguu kabisa, hata kwenda kuswali nishindwe, kijana mbaya sana huyu,” amelala Mzee Tai.

Mzee Tai akaendelea kulalamika kuwa amepata taarifa za ndani kabisa kuwa uamuzi wa kuweka kodi kwenye gesi – asilia inayotumika kwenye magari kake, Daktari Mwigulu Nchemba amemlega mzee huyo ili asiweze kujongea anapotaka kufanya hivyo.

Mzee Tai anasema iweje matumizi hayo yameanza hivi karibuni, na magari yenyewe machache sana, likiwamo lake, wafanyiwe “mtima nyongo” na Daktari Mwigulu Nchemba?

Kwamba kuna vyanzo vingi vya mapato ya serikali, kwanini sasa ang’ang’ane na magari yasiyofika hata 2000 yanayotumia gesi hiyo hadi sasa?

“Mimi naona kabisa ameamua kunimaliza, hata umri wangu hauonei huruma, yeye anasemasema tu bungeni kwamba gari langu sasa nifugie kuku, nitaweza wapi mimi bei ya mafuta yao? Anahoji Mzee Tai huku machozi yakimlengalenga.

Mzee Tai anasema alishasahau kabisa kununua mafuta ya petroli ya Shilingi 15,000, kwani magari kake – kanakotumia gesi-asilia, akiweka mafuta ya Shilingi 5,000, anakwenda Kibaha – kumsabahi mdogo wake, na kurudi kwake Mtaa wa Lumumba bila shida.

Mzee Tai sasa anamuomba Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye humuita “Mama,” aingilie kati kumzuia Daktari Mwigulu Nchemba kutekeleza kodi hii, kwani akiendelea nayo, basi sinia sitizeni huyo ataaga dunia “chap- kwa haraka.”

**Green Horizon**  
Mowing & Lawn Care

# GO GREEN GO CLEAN

Save 20% on your first booking with us!

### OUR SERVICES

- Domestic and Outside Maintenances
- Garden
- Mowing and lawn care
- Pressure Washing
- Tree and hedge trimming
- Landscaping Design
- Garden Renovation

HELPING TO KEEP OUR COMMUNITY CLEAN

0713-821 441  
0672-782 223

Makongo CCM

Mowinandlawn\_care

## Habari

## Nyuma ya Bajeti 2024/25

Na Peter NYANJE,  
Dodoma

**M**ARA baada ya Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba kumaliza kuwasilisha Bajeti ya Serikali bungeni Alhamisi iliyopita, wataalamu wa uchumi walishindwa kuelezea moja kwa moja kuwa ilikuwa ni bajeti ya nini.

Saa kadhaa, baada ya kuchakata namba na kauli zilizotoka kwa Dkt. Nchemba, wachumi na wataalamu wa sekta zingine wameibuka na kuichambua bajeti ya Tanzania kwa mwaka 2024/25.

Kuna mambo ambayo yameshasemwa waziwazi, lakini ukweli wake ukiwa umejificha kwenye namba.

Mathalan, mosi; ukiziangalia namba za kiasi cha fedha cha bajeti na kulinganisha na kile kilichotengwa katika mwaka uliopita, utaona kuwa kiasi cha bajeti kimeongezeka.

Pili, ukisikiliza tu maneno kuwa serikali imetenga fedha kwa ajili ya kulipa madeni unaweza usijue uzito wa suala hilo mpaka utakopojumlisha namba ndipo utabaini kuwa madeni, kwa ujumla wake, yatachukua takribani theluthi moja ya bajeti yote.

Tatu, kupitia bajeti hii, serikali lilenga kutekeleza pendekezo la Benki ya Dunia kuhusu miradi mikubwa kwa kuiwezesha sekta binafsi kutekeleza, badala ya kazi hiyo kufanywa na serikali, lakini hatua zilizochukuliwa katika bajeti hii hazitoshi kutekeleza hilo kwa haraka.

Kuhusu kiasi cha bajeti hii kuizidi ile ya mwaka jana, ni wazi iwapo bajeti hiyo itapimwa kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania, lakini ikipimwa bajeti kwa thamani ya dola ya Marekani, bajeti hiyo imeshuka.

Iko hivi; bajeti ya 2023/24 ilikuwa shilingi trilioni 44.38 ambayo kwa kiwango cha kubadilisha dola wakati huo ilikuwa na thamani ya dola za Marekani bilioni 19.28. Bajeti ya 2024/25 ni shilingi trilioni 49.34, lakini ukiweka katika dola ina thamani ya dola za Marekani bilioni



*Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba akiwasilisha bungeni, jijini Dodoma kwa ajili ya kusoma bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25. (Picha na wizara).*

19.00

Hii nimaanisha kuwa kwa thamani ya fedha za Tanzania, bajeti hii imeongezeka kwa zaidi ya shilingi trilioni 4, ingawa kwa thamani ya dola za Marekani, bajeti imesinyaa kwa dola bilioni 0.28 na hilo halionekani kwenye maneno isipokuwa kwa kuchakata na kulinganisha namba.

Kwa mujibu wa wataalamu wa uchumi, suala la kuiweka bajeti ya serikali kwenye thamani ya dola ni muhimu kwa sababu sehemu kubwa ya ununuzi wa bidhaa nje ya nchi hufanyika kupitia sarafu hiyo ya taifa kubwa la Marekani, na wakati mwingi mashirika na taasisi kubwa za kiuchumi duniani, hupima uchumi wa nchi kwa kutumia dola.

Aidha, suala hilo ni muhimu sasa kutokana na ukweli kuwa ka miezi kadhaa, Tanzania imekuwa ikikabiliwa na uhaba mkubwa wa dola kama ambavyo Waziri Dkt. Nchemba alivyokiri kwenye hotuba yake ya bajeti.

“Kama ilivyokuwa kwa nchi nyingi duniani, nchi yetu pia ilikabiliwa na changamoto ya upungufu wa fedha za kigeni mwaka 2023/24. Changamoto hii ilisababishwa na mambo mbalimbali ikiwemo athari za Covid-19; vita

## Nyuma ya Bajeti 2024/25

*Inatoka Uk. 6*

inavyoendelea nchini Ukraine na katika ukanda wa Gaza; mabadiliko ya tabianchi; na kubadilika kwa sera za fedha katika nchi zilizoendelea,” alisema Dkt. Nchemba.

Hata hivyo, licha ya kukiri kuwepo kwa tatizo hilo, Waziri Nchemba hakuainisha mikakati mikubwa ya serikali kukabiliana na hali hiyo zaidi ya kupiga marufuku malipo kwa kutumia dola kwa mauzo ya ndani ya bidhaa na huduma.

Katika uchambuzi wa bajeti hiyo, kampuni ya ushauri wa masuala ya uchumi na fedha, PwC, nayo inaonyesha umuhimu wa kuwa na mikakati madhubuti ya kuhakikisha dola inapatikana, hasa kwa wanaojihusisha na biashara ya nje.

“Kuna kauli kuhusu hatua zitakazochukuliwa kuzuia matumizi ya dola katika malipo ya bidhaa na huduma kwa biashara za ndani, lakini tunasubiri maelezo ya kina kuhusiana na katazo hili – hasa, iwapo hili litahusisha kuongezea thamani sarafu ya ndani au ni suala pia litakalohusu bei,” inasomeka sehemu ya taarifa ya PwC iliyotolewa muda mfupi baada ya bajeti kusomwa.

**Miradi mikubwa**

Mwishoni mwa mwaka jana katika ripoto yake kuhusu uchumi wa Tanzania, Benki ya Dunia ilitoa ushauri kuhusu utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo.

Benki hiyo ilisema kuwa ni vyema Tanzania ikatekeleza miradi hiyo, lakini kuna umuhimu wa kuishirikisha pia sekta binafsi.

Benki ya Dunia ilibainisha kuwa iwapo sekta binafsi itashirikishwa, itakuwa ni rahisi kujenga na kuimarisha uwezo wa kulipa kodi, lakini serikali yenyewe ikitekeleza miradi hiyo itakuwa inaminyana kukua kwa sekta binafsi.

Kimsingi, serikali ilikubaliana na mapendekezo haya na kuahidi kuyatekeleza na ilitarajiwa kuwa hilo litaonekana kupitia bajeti ya iliyosomwa wiki iliyopita, lakini serikali haikufanya hivyo.

Wataalamu kadhaa wa uchumi wameliambia Pambazuko kuwa ilikuwa ni matarajio yao kuwa kupitia bajeti hii, wangeona jinsi serikali ilivyojiandaa kuishirikisha sekta binafsi katika kutekeleza mitadi mikubwa, lakini kilichoonekana ni serikali kuendelea

*Inaendelea Uk. 15*



**Rais Samia Suluhu Hassan akiwa pamoja na wasaidizi wake wakati akifuatilia Bunge la Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2024/25 kwa njia ya runinga nyumbani kwake, Chamwino, Dodoma. Hotuba hiyo ilikuwa ikisomwa bungeni na Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba. (Picha na Ikulu).**

## Mezani kwa Chahali

Na Evarist Chahali  
evarist@chahali.com



### Tanzania sasa iamke kudhibiti ushoga

**M**IONGONI mwa masuala ambayo yametawala mijadala miongoni mwa Watanzania kwa zaidi ya wiki sasa, ni kuhusu mtandao wa kijamii wa X, ambao zamani ulijulikana kwa jin la Twitter.

Mtandao huo wa kijamii unatuhumiwa kuwa unahamasisha vitendo vilivyo kinyume na maadili ya Watanzania, hususan ngono na ushoga.

Watu mbalimbali wamejitokeza hadharani kuitaka serikali kufungia mtandao wa X. Sauti zinazosikika zaidi ni za baadhi ya viongozi wa dini na wanasiasa.

Hata hivyo, kuna masuala kadhaa ambayo yanapaswa kuwekwa bayana kuhusiana na suala hilo.

Kwanza ni ukweli kwamba hata kabla haujanunuliwa na bilionea, Elon Musk, na kubadilishwa jina kutoka Twitter na kuwa X, mtandao huo wa kijamii umekuwa na maudhui ya ngono ikiwa ni pamoja na ushoga.

Kilichofanyika majuzi ni uongozi wa mtandao huo wa kijamii kuweka bayana sera inayoruhusu maudhui ya ngono ikiwa ni pamoja na ushoga.

Pili, X siyo mtandao pekee wa kijamii wenye maudhui ya ngono ikiwa ni pamoja na ushoga. Yayumkinika kutamka

pasi shaka kwamba mtandao mwingine wa kijamii wa TikTok ni maarufu “mara milioni” zaidi ya X kwenye maudhui ya ngono ikiwa ni pamoja na ushoga.

Na kwa hakika, ukitembelea mtandao huo wa kijamii utakutana na lundo la video za vijana wa Kitanzania wanaojihusisha na ushoga wakijitangaza waziwazi kwamba wao ni mashabiki wakubwa wa vitendo vya ushoga.

Hata hivyo, wengi wa wanaoitaka serikali ifungie mtandao wa X, wapo huko TikTok pia, hawajawahi kutaka hatua zichukuliwe dhidi ya mtandao huo wa kijamii. Huu ni unafiki.

Ileweke kuwa kuna ukweli mmoja muhimu kuhusu mtandao wa kijamii, kwamba, kwa kiasi kikubwa, mtumiaji huona kile tu anachotaka kukiona.

Mitandao ya kijamii imekuwa kama hali halisi ilivyo mtaani. Kwa mfano, mtu anayetaka kufanya ibada hatarajwi kwenda baa, bali kanisani au msikitini.

Kadhhalika, kwenye mitandao ya kijamii, mtu anayetaka kuona habari za siasa au uchumi, hatarajwi kwenda kwenye akaunti zenye maudhui ya ngono.

Kadhhalika, kwenye suala la ushoga, kuna tofauti za kimaadili kati ya nchi za Magharibi, hususan Ulaya na Marekani na Tanzania.

Kwa nchi nyingi za Magharibi, ushoga siyo tu ni halali, bali ni haki ya binadamu ilhali ni haramu na kinyume cha sheria nchini Tanzania.

Kwamba ngono na ushoga vimetapakaa zaidi mitaani kuliko huko X, lakini “askari wa maadili” wapo kimya kuhusu hilo.

Wito wangu kwa serikali ni kutumia busara katika kushughulikia suala hili ili kuokoa kizazi kinachoonekana kupotea kwa kuendekeza masuala ya ngono na ushoga.

Tamke sasa.

Unaweza kuwasiliana na mwandishi kwa email hii: [evarist@chahali.com](mailto:evarist@chahali.com)



Dkt. Dorothy Gwajima - waziri anayehusika na maadili kwa Watanzania.





## Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

### Bodi ya Mikopo isigeuke kero nyingine

Na Rashid MTAGALUKA

**M**UDA siyo mrefu kutoka sasa, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HELSB) nchini Tanzania itatangaza kufungua dirisha lake la kupokea maombi ya mikopo ya elimu kutoka kwa wanafunzi .

HELSB imekuwa ikitoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa nia ya kuwezesha kupatikana kwa elimu kwa wote hapa nchini.

Hata hivyo, tangu mwaka 2021, kumekuwa na mabadiliko katika asilimia za mikopo inayotolewa, hasa katika pesa za ada (tuition fees).

Siyo utani, mabadiliko haya yameleta changamoto kwa wanafunzi, wazazi na walezi, hususan wale wanaotoka familia masikini.

Hali ilivyo ni kwamba, HELSB imepunguza kiasi cha pesa za ada kinachotolewa kwa wanafunzi. Mfano, kwa kozi yenye ada ya Shilingi 1,200,000, mwanafunzi anaweza kupewa Shilingi 600,000 au wengine kiasi kidogo zaidi kinachoweza kufika Shilingi 250,000.

Hali hii inawalazimu wazazi kufidia kiasi kinachobaki, jambo ambalo ni gumu hasa kwa wazazi wa kipato cha chini.

Wazazi wakulima ambao wanategemea mazao ili kupata fedha, wanapata changamoto kubwa zaidi, hasa msimu unapokuwa mbaya, kwa maana ya kukosa mazao ya kutosha.

Hivyo, baadhi ya wanafunzi wanajikuta wakitumia pesa zao za kujikimu (boom) kuongeza kwenye ada, hali inayowafanya waishi kwa shida.

Baadhi ya wanafunzi, hususan kina dada, tunawashuhudia wakiingia, bila kupenda, kwenye biashara zisizo rasmi ili kujikimu, jambo ambalo linaweza kuathiri elimu na usalama wao.

Hoja yangu hapa kwanza ni kuiomba bodi iangalie uwezekano wa kulipia ada kwa asilimia 100, hii itawasaidia wanafunzi kuzingatia masomo yao badala



*Prof. Adolf Mkenda - Waziri wa Elimu*

ya kuhangaika kutafuta fedha za ada.

**Pili**, mikopo inapaswa kugawiwa kwa kipaumbele kwa wanafunzi wanaotoka familia masikini; hii inaweza kufanywa kwa kutumia taarifa za kipato za wazazi na familia husika.

**Tatu**, kwa kuwa serikali ina changamoto za kifedha, inaweza kuwaacha wazazi wawe wanatoa hela za matumizi ya bweni na kujikimu kwa watoto wao badala ya ada nzima. Hii itakuwa rahisi zaidi kwa wazazi kulipa.

**Nne**, serikali inaweza kushirikiana na sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali kuongeza mfuko wa mikopo na misaada kwa wanafunzi.

Na jambo jingine ni kuweka utaratibu wazi na wa haki katika utoaji wa mikopo ili kila mwanafunzi mwenye sifa apate mkopo. Uwazi huu utapunguza malalamiko na kuimarisha usawa.

Ni muhimu kwa bodi na serikali kutafakari upya mfumo huu na kufanya maboresho yanayolenga kusaidia vijana wa Tanzania.

Kuwekeza kwenye elimu ni kuwa na uhakika wa maendeleo siyo kwa familia tu, bali taifa zima.

*Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu namba: 0784 438 546 na email: ; mtagaluka@gmail.com*

## Habari

### Mchumi: Kodi gesi ya magari iondolewe

Na Mwandishi WETU

**S**ERIKALI imetakiwa kufikiria upya – na ikiwezekana kuachana na uamuzi wake wa kuanza kutoza kodi gesi asilia inayotumika kuendeshea magari kwani uamuzi huo utakuwa na athari hasi kwenye uchumi.

Akiwasilisha bajeti ya Tanzania kwa mwaka 2024/25, wiki iliyopita bungeni jijini Dodoma, Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba alitangaza kuanzishwa kwa kodi hiyo.

Alisema serikali inakusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta - Sura 220 ili kuanza kutoza Shilingi 382 kwa kila kilo ya gesi asilia inayotumika kwenye magari.

Dkt. Nchemba alisema hatua hiyo inalenga kukusanya fedha ambazo zitatumika kwenye matengenezo ya barabara pamoja na kuleta usawa kwa kuwa magari yanayotumia mafuta, tayari yanachangia mapato kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya barabara.

Hata hivyo, mtaalamu wa uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dkt. Wilhelm Ngasamiaku amesema pamoja na nia nzuri ya serikali, lakini hatua hiyo inaweza kuwa na athari hasi kwa uchumi, hivyo kushauri iondolewe kwa sasa.

Alibainisha kuwa suala la matumizi ya gesi limekuwa kimbilio kwa wenye magari, badala ya mafuta na kwa kiasi kikubwa ni moja ya mambo ambayo yanashusha kidogo ukali wa gharama za maisha.

Dkt. Ngasamiaku amesema serikali yenyewe ndiyo iliyoamua kuanzisha matumizi ya gesi asilia iliyoshindiliwa ili kutumika kwenye magari kama njia ya kupunguza gharama miongoni mwa wanaoendesha magari.

Amesema kwa kuwa ndio kwanza watu wanaanza kutumia gesi kwenye magari badala ya mafuta, haitakuwa vyema kuanza kuweka vikwazo kwenye



*Dkt. Ngasamiaku*

utaratibu huo kwa kuwawekea kodi.

Amebainisha matumizi ya gesi kwenye magari kuwa uyanashusha gharama na kufanya watu wengi kumudu kuwa na usafiri wa uhakika, lakini bidhaa hiyo itakapofanywa kuwa aghali kwa kuongeza kodi, basi itakuwa vigumu watu wengi kumudu.

“Inaweza kufika mahali gharama za mafuta zikawa sawa na zile za gesi kwa hiyo gesi haitakuwa na ahueni yoyote katika kushusha gharama za maisha,” ameongeza.

Kutokana na ongezeko hilo, bei ya kilo moja ya gesi kwenye magari inaweza kupanda kutoka kiwango cha sasa cha Shilingi 1,932 kwa kilo, hadi shilingi 2,314.

Amesema kuwa ongezeko la kodi kwa gesi asilia – hasa inayotumika kwenye magari, kwa upande mwingine, ni hatua inayopingana na dhamira na juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kuhimiza matumizi ya nishati salama nchini Tanzania na hata Bara la Afrika.

“Tunapoenda kwenye vyanzo vya nishati safi, tunapunguza uzalishaji wa hewa ukaa. Tunapotumia gesi kwenye magari tunapunguza uzalishaji wa hewa chafu, sasa tukianza kuweka kodi kwenye nishati safi, tunasababisha kuongezeka kwa hewa ukaa kwa sababu watu wataendelea kutumia vyanzo vichafu vya nishati,” amesema msomi huyo.

## TPA yachochea maendeleo kwa gawio nono



*Rais Samia Suluhu Hassan akipokea mfano wa hundi yenye thamani ya Shilingi bilioni 153.9 kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Placeduce Mbossa, ikiwa ni gawio la mamlaka hiyo kwa serikali. (Picha na IkuLu).*

### Na Mwandishi WETU

**O**NGEZEKO la Shilingi bilioni 153.9 katika Hazina ya serikali, ni fedha nyingi ambazo zinaongeza kasi na msukumo wa kazi za maendeleo na kuleta mageuzi makubwa kwa umma, endapo zitatumika vyema.

Kiasi hicho cha fedha, endapo kitaingizwa katika ujenzi wa barabara pekee, basi Tanzania itakuwa imeongeza kilomita zaidi ya 154 za mtandao wake wa barabara za lami.

Fedha hizo zinaelezwa na wachumi na wadau wa maendeleo kuwa zinaweza kupunguza makali ya uhaba wa dawa na vifaa tiba kwa kiasi kikubwa na kusaidia kupunguza vifo vinavyosababishwa na kukosekana kwa bidaa hizo katika hospitali.

Sasa basi, kiasi hicho cha fedha, wiki iliyopita, kimepokelewa na serikali kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), ikiwa ni gawio lake kwa mwaka 2023/24.

Fedha hizo inaelezwa kuwa ni sehemu ya matunda ya maboresho ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na kampuni mbili za kimataifa katika Bandari ya Dar es Salaam pekee.

Kutokana na gawio hilo, TPA imevunja

rekodi kwa kutoa kiasi hicho cha fedha kwa serikali na kuibuka kina miongoni mwa mamlaka na mashirika ya serikali yaliyotoa gawio.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Prasureduce Mbossa, ameliambia Pambazuko kwamba gawio hilo kwa serikali, kwa kiasi hicho kikubwa ni matunda ya uwekezaji uliofanywa katika Bandari ya Dar es Salaam.

TPA imefanya uwekezaji mkubwa kwa kuboresha miundombinu ya kwa bandari zake. Katika Bandari ya Dar es Salaam, TPA imefanya maboresho ya ujenzi wa magati na kuongeza kina, imetanua lango la kuingilia bandarini na sehemu ya kugeuzia meli.

Mamlaka hiyo pia imekuwa ikishirikiana na vyema kiutendaji na wawekezaji ambapo hadi sasa Kampuni ya DP World imeshafanya uwekezaji mkubwa kwa kununua vifaa kama SSGR (Ship to Shore Gang Cranes) nane (8), pamoja na T.T. (Terminal Tractors) 50.

Kutokana na uwekezaji huo na maboresho mengine yanayoendelea kufanywa, Bandari ya Dar es Salaam sasa imekuwa ya kisasa zaidi na inaendelea kuongeza ufanisi na kutoa huduma zake za kuhudumia meli na mizigo kwa ubora na ufanisi zaidi.

## Habari

## Wengi wahoji: “Bajeti ya nini kwetu?”

Na Waandishi WETU

**P**AMOJA na umuhimu wa bajeti ya nchi kwa wananchi, wengi bado hawana mwamko wa kuifuatilia wakati ikiwasilishwa bungeni.

Wapo pia wanaohoji umuhimu wa bajeti hiyo kwa mtu binafsi kwa maelezo kwamba haiwasaidii “kupata ugali wao wa kila siku.”

Hali hiyo imethibitishwa na gazeti la Pambazuko wiki iliyopita, Alhamisi – Juni 13, wakati Waziri wa Fedha wa Tanzania, Dkt. Mwigulu Nchemba alipokuwa akiisoma Bungeni, Dodoma.

Pambazuko limehoji wananchi 61; wanaume wakiwa 56 na wanawake watano katika maeneo ya Kijitonyama, Sayansi, Mwenge na Sinza – yote ya Dar es Salaam, ambapo wengi wanadai hawawezi “kupoteza muda wa kusikiliza kitu kischowasaidia.”

Kati ya wanaume 56, ni saba tu ndiyo angalau walionekana kuwa na taarifa za kuwepo siku ya kusoma bajeti, huku waliobaki wakisema “hawana habari hizo.” Wanawake wote watano walisema

“hawajui kuwepo kwa siku hiyo.

Hatua hii ya kususa kufuatilia bajeti inaposome kwa mara ya kwanza Bungeni, sasa imejengeka zaidi, hasa kwa “wananchi wa kawaida,” ambao wengi wamekutwa wakiendelea kufanya shuguli zao, ama kuwa mbele ya redio na televisheni wakifuatilia “mambo mengine” wakati ni muda wa bajeti kuwasilishwa.

Hii ni tofauti na miaka ya nyuma ambapo siku ya bajeti lilikuwa ni tukio kubwa ambalo lilisimamisha karibu shughuli zote ili watu wapate nafasi ya kufuatilia kwa karibu mapendekezo ya mapato na matumizi ya serikali ya mwaka wa fedha husika.

Mojawapo ya vivutio vikubwa vya siku ya kusomwa bajeti enzi hizo ilikuwa ni kuhisi kuwepo suala la nyongeza ya mishahara kwa wafanyakazi, utamaduni ambao umetoweka katika bajeti za miaka ya hivi karibuni.

Wakati huo serikali ilikuwa na utamduni wa kutangaza mabadiliko ya kima cha chini cha mishahara ya sekta ya

Inaendelea Uk. 13



## Wengi wahoji: “Bajeti ya nini kwetu?”

*Inatoka Uk. 12*

umma kila mwaka mpya wa fedha.

Kupanda kwa mishahara haikuwa neema kwa wafanyakazi wa umma tu, bali pia hata kwa makundi mengine mengi na karibu maeneo yote ya kijamii na kiuchumi yanayoguswa moja kwa moja na matumizi ya wafanyakazi.

Kama huamini kuwa watu wengi siku hizi – wakati wa kusomwa kwa bajeti na hata kufuatilia bajeti yenyewe si muhimu sana kwao, fanya tu utafiti mdogo wa haraka kwa kuwauliza ndugu, jamaa na marafiki kama walimsikiliza Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba, alipofanya wasilisho la Bajeti ya Mwaka 2024/25 bungeni Juni 13 mwaka huu.

Pambazuko lilifanya hivyo wakati bajeti inasomwa Bungeni jijini Dodoma na waandishi wetu walikuwa wakizunguka maeneo mbalimbali kuangalia mapokeo ya tukio hilo miongoni mwa wananchi wa kawaida.

Utafiti huo mdogo iligundua kuwa wapo watu ambao hata hawakufahamu kuwa siku ile ilikuwa ni siku ya kusomwa kwa bajeti ya nchi.

Wapo waliokuwa wanafahamu, lakini hawakujua mambo kwa undani hata kwa suala la ukubwa wa bajeti kuwa ni ya shilingi trilioni 49.3 ambazo nyingi zitatokana na kodi watakazolipa.

“Mapato ya ndani yanakadiriwa kuwa jumla ya shilingi trilioni 34.61, sawa na asilimia 70.1 ya bajeti yote na asilimia 15.7 ya Pato la Taifa. Kati ya mapato hayo, mapato yatakayokusanywa na Mamlaka ya

Mapato Tanzania (TRA), yanakadiriwa kuwa shilingi trilioni 29.41” alisema Dk. Nchemba wakati akiwasilisha bajeti hiyo.

Wanazuoni hususani wale wa masuala ya kijamii na kiuchumi, wanasema zipo sababu nyingi kwa nini watu hawana mwamko wa kusikiliza bajeti.

Wanaitaja moja ya sababu hizo kuwa ni uandaaji wa bajeti kutokuwa shirikishi tangu hatua za awali.

Sababu nyingine ni bajeti kutokuwa

na majibu ya moja kwa moja kwa changamoto zinazowakabili watu wengi wa kawaida hasa ukali wa maisha.

“Mfumo wa kisheria na utaratibu wa kutengeneza bajeti hauwashirikishi wananchi wa kawaida, bali inaandaliwa na watendaji wa serikali pamoja na wataalamu wake,” Mchumi Mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Bravious Kahyoza, ameliambia Pambazuko juzi – Jumamosi alipoulizwa tatizo ni nini.

“Sababu nyingine ni wananchi wanaona kuwa bajeti imekuwa ni sehemu tu ya watu wachache wanaofaidika na keki ya taifa kwa vile wameshuhudia kwa miaka mingi pamoja na bajeti kuwepo, lakini wameendelea kuwa maskini,” aliongeza na kueleza kuwa Tanzania ni tofauti na baadhi ya majirani zake.

Akifafanua, mwanazuoni huyo alisema Tanzania iko nyuma ikilinganishwa na Kenya na Rwanda linapokuja suala la wananchi kufuatilia na kushirikishwa kwenye kuandaa bajeti za serikali.

Siku ya bajeti maeneo mengi yaliyotembelewa na waandishi wa gazeti hili walishuhudia watu wengi wakiendelea na shughuli zao huku televisheni kwenye migahawa na baa zikionyesha mechi za mpira wa miguu na tamthilia. Hali hiyo ni tofauti na nchi za Kenya na Rwanda.

Hotuba za bajeti katika nchi hizo zilikuwa zinafuatiliwa kwa umakini kweli kweli. Bajeti kwa nchi za Afrika Mashariki husomwa siku moja.

“Wananchi wanaona wanapoteza tu muda wao maana hata huko nyuma walipofuatilia wameendelea kuwa maskini halafu kodi zinazidi kuongezeka kila mara na kufanya maisha yawe magumu zaidi,” ameongeza Dkt. Kahyoza.

Mkazi wa Bungo, Kibaha, mkoani Pwani, Joseph Chigana, anasema yeye alikuwa kanisani, lakini ana kumbukumbu mara ya mwisho kufuatilia bajeti ilikuwa lini wakati miaka ya nyuma

## Habari

## Wengi wahoji: “Bajeti ya nini kwetu?”

Inatoka Uk. 13

alikuwa hapitwi kabisa na tukio hilo.

“TV hazikuwepo wakati huo, lakini tulikusanyika kusikiliza redio kuhusu nini serikali imekipanga na jambo kubwa lilikuwa ni matarajio ya nyongeza za mishahara,” alisema.

Katika meneo mengi ya Kijitonyama, Dar es Salaam, ambapo Pambazuko lilipita, watu wengi walionekana kutokuwa na mwamko wa kufuatilia bajeti iliyokuwa ikiendelea kusomwa bungeni mjini Dodoma.

Wakati bajeti ikiendelea kusomwa majira ya saa 11.30 jioni, waandishi wetu walishuhudia wananchi wakiendelea kuangalia mpira katika baa zenye wateja wengi na maeneo mengi kama hayo.

Hii ni tofauti na miaka ya nyuma ambapo wananchi walikuwa wakiacha shughuli zao na kufuatilia bajeti katika maeneo jirani, kama wafanyavyo kunapokuwa na mechi za mpira wa miguu katika kipindi hiki.

“Mimi hata sijui kama kuna bajeti inayosomwa leo, kwanza inanisaidia nini? Mimi tangu nilipoamka asubuhi ninahangaika kutafuta chakula cha watoto wangu, muda huo wa kufuatilia ulaji wa watu naupata wapi,” alisema mwananachi aliyejitambulisha kwa jina la Yahaya Hassan.

Mmoja wa wafanyabiashara katika

eneo la Makumbusho, Hamisa David, alisema hana muda wa kufuatilia kwa sababu haoni kama kuna jipya zaidi ya kuendelea kuwabana wananchi kwa kodi.

Mfanyabiashara mdogo ambaye hakupenda kutaja jina lake alisema hajui lolote kuhusu kusomwa kwa bajeti na kuwa kwake yeye haoni kama inamhusu, kwa kuwa hajui inamsaidia nini.

“Kusema kweli sikuisikiliza kwa sababu sijui wala kuona faida yake ni nini katika maisha yangu haya ambayo ni magumu sana,” alieleza Faudhia Ibrahim, mkazi wa Mtwara.

## Wapo waliofuatilia

Dkt. Clay Maro wa Iringa naye anasema hakuisikiliza, lakini hiyo ilitokana na kutingwa na majukumu.

Mwalimu Lucas Oganje wa Mwanza aliisikiliza kwa ufupi na amesema ana imani kuwa itasaidia kuinua hali za maisha nchini.

Alisema bajeti hiyo imeweka malengo ambayo yakitekelezwa ipasavyo itasaidia kuinua hali ya maisha.

Mkazi wa Sinza, Dar es Salaam, Lightness Raymond, aliyekutwa kwenye duka lake la dawa akifuatilia bajeti alisema kuna haja kwa jamii nzima kujua umuhimu wa bajeti kwani huo ndio mwongozo wa nchi katika mwaka husika wa fedha.



## Nyuma ya Bajeti 2024/25

### Inatoka Uk. 7

kujimilikisha utekelezaji.

“Tulitarajia kuona masuala ya PPP (ushirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi), ukipewa kipaumbele, lakini hilo halionekani sana kwenye bajeti...”

“... Ni kweli kuwa kuna aina fulani ya upendeleo kwa sekta binafsi kupitia kodi na ushuru ambao kwa kiasi kikubwa haijaguswa au kupandishwa, lakini hiyo ni hatua ndogo sana ukilinghanisha na kile kinachotakiwa kufanyika ili kuiwezesha sekta binafsi kushiriki kwenye miradi hii,” amesema Dkt. Lenny Kasoga, mchambuzi wa masuala ya uchumi.

Ni kweli kuwa katika bajeti ya mwaka huu, serikali haijaongeza kodi na ushuru kwenye maeneo mengi ya wazalishaji, lakini ilitarajiwa kuwa kuwe na vivutio zaidi kwa sekta ya uzalishaji jambo ambalo bajeti halijalifanya kwa kiasi kikubwa.

### Ni bajeti ya kulipa madeni

Waziri Dkt. Nchemba amejitahidi kueleza kuhusu deni la taifa na kukiri kuwa limeongezeka kwa kiasi kikubwa na akaeleza sababu kwa nini deni limekua kwa kiasi hicho.

Wachumi wengi hawana tatizo na nchi kukopa kwani ndio utaratibu unaotumika na nchi nyingi duniani kutekeleza mambo yake.

Lakini, hoja ipo kwenye aina ya mikopo kwa maana ya masharti yake na jinsi inavyotumika.

Serikali imekuwa ikisema tu kuwa mikopo inachukuliwa ili kutekelea miradi mikubwa ya kimkakati, lakini haisemi bayana iwapo mikopo hii ina masharti ya aina gani.

Hili ni muhimu kulifahamu kwa sababu masharti mengine yanawexa kuiweka nchi mahali pabaya.

Mathalan, mikopo ya kibiashara ambayo ina riba kubwa na muda mfupi wa kulipa. Iwapo serikali inachukua mikopo ya aina hii ni vyema aikaeleza ili wananchi wajue.

“Serikali inakopakopa tu, hata hayo maendeleo hatuyaoni badala yake maisha yanazidi kuwa magumu kila kitu kinasuasua, halafu wanatambia deni la serikali hilo ni deni letu kwa sababu sisi wananchi ndio walipaji,” anasema Hellen Kijo Bisimba, Mkurugenzi wa zamani wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Lakini jambo mbalo hajiaelezwa waziwazi kwenye bajeti ni kuwa sehemu kubwa ya bajeti itatumika kulipa madeni.

Kwa ujumla wake, kiasi cha Shilingi trilioni 15 kimetengwa katika bajeti kwa ajili ya kulipa madeni.

Kiasi hiki ni karibia theluthi moja ya bajeti yote na inaelezwa na wanazuoni kuwa ni “kiasi kikubwa mno.”

Inamaanisha kuwa kwa ujumla wake, Shilingi trillion 15 za kulipa deni ukiongeza matumizi ya lazima ya serikali (first charge) unapata jumla ya zaidi ya shilingi trilioni 26.

Hii ina maana kuwa makusanyo yote ya kodi ya shilingi trilioni 22 hayatoshi kugharamia malipo ya madeni na matumizi muhimu ya serikali (hasa mishahara) kwa pungufu ya shilingi trilioni nne.

Iwapo suala la kushuka kwa thamani ya shilingi litatiliwa maanani, hapo utabaini kuwa sehemu kubwa ya bajeti ya Tanzania, hasa katika fedha za maendeleo na sehemu ndogo ya matumizi ya kawaida, itategemea mikopo na misaada.

Hii siyo hali ya kuridhisha kwa nchi kama Tanzania ambayo inapigana kukuza uchumi wake.

“Tuepoke kukopa holela, Tusikope tu eti kwa sababu wakopeshaji wapo. Tunahitaji pia nidhamu katika matumizi ya fedha zitokanazo na mikopo hiyo pamoja na fedha nyinginezo...”

“... Fedha zilizokopwa sharti zitumike tu katika shughuli zinazotuzalishia faida na kukuza uchumi,” anashauri Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. George Kahangwa.

**Makala****Bajeti kudhibiti uhaba, bei ya sukari**

Na Martin KUHANGA,

**K**ARIBU kila mwaka, Tanzania, hasa Bara, imekuwa ikikabiliwa na uhaba mkubwa wa sukari, hivyo kusababisha bei ya bidhaa hiyo kupanda kwa kiasi kikubwa.

Malalamiko ya kuadimika kwa sukari kutoka kwa wananchi ni makubwa kwa sababu uhaba huo huambatana na kupanda kwa bei, huku upatikanaji wake ukiwa haba.

Uhaba huo haelezwi kinagaubaga, na hutolewa sababu zisisokuwa na mashiko. Kwa mfano, sukari ilipoadimika kwa mara ya mwisho, Januati mwaka huu, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema uhaba wa sukari nchini ulisababishwa na mvua nyingi zilikokuwa zikiendelea na kusababisha viwanda vya sukari kushindwa kuzalisha kwa kiwango kinachotakiwa.

Kutokana na uhaba huo, Bashe alitangaza kuchukuliwa kwa hatua kadhaa kuhakikisha uhaba wa sukari unaondoka, haraka iwezekanavyo.

Miongoni mwa hatua alizotangaza ilikuwa ni pamoja na kutoa vibali vya kuruhusu uingizaji wa sukari wa takriban tani 100,000 kutoka nje.

Bashe alitoa taarifa baada ya bidhaa hiyo muhimu kupanda bei kutoka kutoka kati ya shilingi 2,500 na 2,800 kwa kilo, hadi kati ya shilingi 4,000 hadi 5,000, na katika baadhi ya maeneo, sukari iliadimika kabisa.

Pamoja na hatua hiyo ya serikali, bei ya sukari haikushuka kwa kiwango kilichokuwa kimeelekezwa na serikali (bei elekezi) cha kati ya shilingi 2,500 na 2,800 kwa kilo moja.

Kauli kama hiyo imewahi kutolewa

February, mwaka huu na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Bungeni jijini Dodoma, wakati akijibu swali la Mbunge Stella Manyanya, kuhusu kuadimika kwa sukari nchini.

Waziri Mkuu alikiri kuwepo kwa uhaba wa sukari nchini alioesema ulisababishwa na mvua nyingi zilizonyesha kwenye maeneo kunakolimwa miwa inayotumika kutengeneza sukari, hivyo kuathiri uzalishaji.

Waziri Mkuu alisema serikali imetoa kibali kwa Bodi ya Sukari Tanzania kuagiza sukari kutoka nje ya nchi ili kuwaondolea wananchi, adha ya upungufu wa sukari.

Pamoja na hatua hizo za kuagiza sukari kutoka nje, bado sukari iliyoletwa haikutosha kwa sababu baadhi ya

wafanyabiashara kuficha shehena na kwa waliokubali kuitoa, hawakuiiza kwa bei elekezi kwa madai kuwa waliinunua kwa bei ya juu.

Ifahamike kuwa muda ambao sababu hii ya mvua kubwa ikitolewa, ilikuwa ni wakati wa msimu wa viwanda kuanza kuzalisha sukari haujaanza.

Kwa kawaida msimu wa viwanda kuzalisha sukari huanza mwezi Mei na Juni.

Kinachosemwa ni kuwa kuna hujuma inafanywa na baadhi ya wafanyabiashara kwa lengo la kujipatia faida katika bidhaa hiyo ambayo haizalishwi kwa kiwango cha kutosheleza mahitaji ya nchi.

Na kwa kuonyesha ukweli wa hilo, serikali iliendesha msako katika maeneo mbalimbali nchini, na baadhi ya wafanyabiashara walikamatwa wakiwa na shehena kubwa ya sukari katika maghala ya.

Inaaminika kuwa wafanyabiashara hao walinunua sukari ile iliyopatikana kupitia



**Waziri wa Kilimo,  
Hussein Bashe**



## Bajeti kudhibiti uhaba, bei ya sukari

*Inatoka Uk. 16*

mpango wa serikali kuionusu nchi na uhaba wa sukari.

Hali hiyo na malalamiko ya wananchi kutokana na adha ya uhaba wa sukari kila mwaka, huenda ndiyo yaliyosababisha serikali, katika Bajeti Kuu ya Mwaka wa Fedha 2024/25, kupendekeza hatua za kukabiliana na uhaba wa sukari, unaochochea kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo.

Akiwasilisha bajeti hiyo Bungeni Alhamisi iliyopita - Juni 13, 2024, Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, alipendekeza kufanyika kwa marekebisho katika Sheria ya Sukari Namba 6.

Mapendekezo hayo yalihusu marekebisho katika Sheria ya Sukari Namba 6 ili kuiwezesha Wakala wa Hifadhi ya Chakula (NRFA) kununua, kuratibu na kuhifadhi pengo la sukari kwenye hifadhi ya chakula ya Taifa.

Aidha, Nchemba alipendekeza marekebisho katika kanuni ya NRFA kwa kuijumuisha sukari kuwa sehemu ya Usalama wa Chakula, na tatu kutoza shilingi 50 kwa kilo katika mabaki yanayotokana na uzalishaji.

Hatua hii iliyochukuliwa na serikali inapaswa kupongezwa kwani iwapo itatekelezwa ipasavyo, itasaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti kuadimika kwa sukari katika soko, kunakotokana na uzalishaji mdogo viwandani au hujuma ya baadhi ya wafanyabiashara.

Ikiwa mapendekezo hayo ya serikali yatapita NRFA itakuwa na wajibu wa kununua, kutaratibu na kuhifadhi sukari ili kukabiliana na upungufu wowote utakajitokeza.

Kwa sababu hiyo, sukari itapatikana nchini wakati wote, na kama kulikuwa na wenye viwanda 'wajanja' waliokuwa wakihodhi sukari, itakuwa mwisho wao.

Lakini pia mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni ya NRFA ili kuijumuisha sukari kuwa sehemu ya



**Sukari**

Usalama wa Chakula yakipita, sukari itakuwa ni kati ya bidhaa muhimu zitakazoratibiwa kwa karibu.

Bila shaka, sasa kila taasisi itakayoguswa katika mapendekezo ya serikali, itachukua jukumu la kutekeleza wajibu wake, kuhakikisha sukari inapatikana wakati wote.

NRFA, yenye jukumu la kununua nafaka kwa ajili ya akiba ya chakula kwa taifa ili kukabiliana na majanga yanayoweza kujitokeza, itafanya hivyo pia kwa sukari.

Bodi ya Sukari nayo itatekeleza wajibu wa kuhakikisha kunakuwa na maendeleo ya kutosha katika sekta ya uzalishaji wa sukari nchini kama ilivyopendekezwa na serikali katika marekebisho ya sheria ya bidhaa husika.

Marekebisho hayo ni kutoza shilingi 50 kwa kilo katika mabaki, yatatupatia fedha za kuiwezesha Bodi ya Sukari kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Majukumu hayo ni pamoja na kuendeleza mafunzo na kukuza ujuzi katika sekta ya sukari na kusimamia uzalishaji wa sukari nchini kupitia upanuzi wa viwanda vilivyopo na kuhamasisha uwekezaji mpya.

Aidha, Bodi itasimamia na kuhakikisha kuwa viwanda vya sukari nchini vinazalisha sukari kulingana na uwezo wao na kamwe kusiwepo ujanjaujanja wa kuficha sukari.

## Hoja Binafsi

### Hili la ulawiti linageuka desturi. Tumelaanika!

Na Mwandishi MAALUM

**K**ILA binadamu anavyo viungo vya mwili 78 vinavyogawanyika katika makundi tofauti yanayounda mifumo 10 ya utendaji wa kimwili.

Kuna mifumo ya neva, tezi, mkojo, chakula, ngono, hewa, damu, kingamwili, mifupa, na mfumo wa misuli. Kila mfumo hutenda kazi zake kulingana na kanuni za maumbile asilia.

Lakini sasa, kuna taarifa mbaya zinazoonyesha kwamba baadhi ya Watanania wanatumia mfumo wa chakula kana kwamba ni mfumo wa ngono kwa sababu tofauti. Kati ya 2018 na 2022 matukio 6,771 ya aina hii yamerepotiwa Polisi.

Hii ni idadi kubwa na hakika inatisha. Na tukio la hivi karibuni la mkuu wa mkoa mmoja kulawiti mwanafunzi wa chuo kikuu huko Mwanza, linarefusha orodha hii.

Tukio hilo la mkuu wa mkoa linadaiwa kutokea Juni 2, 2024 ndani ya gari eneo la baa iitwayo “The Cask Bar & Grill,” iliyoko Jiji la Mwanza.

Siku iliyofuata, mwanafunzi huyo anaelezwa kuripoti tukio hilo kwa Jeshi la Polisi, akiielezea kubakwa kwa kulawitiwa na kwamba na uchunguzi wa kitabibu – kutoka kwa daktari, ulithibitisha kuwepo kwa majeraha.

Tukio hilo liliripotiwa na vyombo vya habari tangu Juni 11, 2024, huku gazeti la Mwananchi likiliripoti kwa siku mbili mfululizo.

Wakati huohuo, barua inayodaiwa kuandikwa kwa mkono wa mwanafunzi

huyo, inayoonyesha kuwa na tarehe 6 Juni, 2024, iliubuka mitandaoni, ikionyesha kuwa alikuwa ameama kuondoa kesi hiyo Polisi.

Hata hivyo, katika hatua ya kushangaza, Jeshi la Polisi, kabla ya kusambaa kwa taarifa hizi, lilikuwa kimya, wakati taarifa za tukio hilo zikiwa mikononi mwao.

Katika hali hiyo ya ukimya, wadau mbalimbali walitoa maoni yao, baadhi wakilaani mtuhumiwa, huku wengine wakitilia shaka uhalisia wa taarifa hiyo.

Baadhi ya wadadisi walikwenda mbali zaidi kwa kuandaa dokezo la kisera kwa ajili ya kushughulikiwa na Baraza la Mawaziri, chini ya unyenekiti wa rais.

**D o k e z o**  
la kisera linathibitisha kitafiti kuenea kwa ubakaji wa kilawiti Tanzania na udhaifu wa sheria zilizopo

kupambana na uhalifu huo.

Dokezo linakosoa udhaifu katika mfumo wa sheria ya makosa ya jinai, likipendekeza mageuzi ya kisheria yanayotambua ubakaji wa kilawiti kama shambulio la kimwili, bila kujali jinsia za wahusika.

Aidha, dokezo la kisera linasisitiza umuhimu na uharaka wa marekebisho ya kisheria ili kuhami haki za waathirika wa ubakaji wa kilawiti.

Pia linazitaka asasi za kiraia, vyama vya siasa na serikali kutoa elimu kwa umma juu ya tofauti kati ya mfumo wa ngono na mfumo wa chakula.

Hakika, kwa ongezeko la matukio haya, Tanzania inaelekea kulaanika, ikiwa bado haijafika huko.



*Sheria*

## 'Rais bora ambaye sasa hawezi kutokea'

Na Golden MATONGA,  
Lilongwe

**NYOTA** ya mwanasiasa kijana wa Malawi, Saulos Chilima imekuwa iking'ara kiasi cha kutisha kila kiongozi anayekuwa madarakani.

Kutokana na kupendwa na kukubalika kwa wananchi wa Malawi, hisia kwamba Chilima atakuja kuongoza nchi hiyo, hazikuishia miyoyoni mwa watu, bali zilikuwa zikianikwa wazi kupitia mitandao ya kijamii; Facebook, X, Instagram na maeneo mengine ya kupashana habari.

Hata hivyo, matamano ya watu wa Malawi kumhusu Chilima, sasa yamepotea. Kiongozi huyo hayupo. Amefariki dunia kwenye ajali ya ndege.

Habari za kifo cha makamu huyo wa rais katika ajali ya ndege zimeleta taharuki na zaidi sana, majonzi kwa umma wa Malawi na wengine wengi nje ya mipaka ya nchi hiyo.

Hakuna mtu mwingine nchini Malawi ambaye aliweza kuruka viunzi vya ukabila, ukanda, uwezo wa kifedha na rangi kama Saulos Chilima.

Baada ya kuwa na manaibu marais wawili; wa kwanza akiwa Peter Mutharika, na kisha Lazarus Chakwera - iliaminika kwamba sasa Chilima ndiye anayefuata kuwa mkuu wa nchi.

Chilima ambaye alikuwa mchapa kazi na mwenye sera, ndiye alikuwa uso wa kiteknolojia wa serikali ya sasa. Sifa yake akiwa kiongozi wa mabadiliko ilianza enzi zake za ajira, akiwa mkurugenzi mkuu wa Airtel, kampuni ya kubwa ya mawasiliano nchini humo.

Profesa Blessings Chimsinga, ambaye aliwahi kuwa waziri katika baraza la mawaziri pamoja na Chilima, anaeleza kwamba atamkumbuka mfanyakazi mwenzao ambaye alijikita kwenye masuala badala ya siasa za kuchafuana na umimi.

"Alifanikiwa kueneza wazo la kujenga Malawi ambayo ingesaidia kusambaza



**Saulos Chilima**

matunda ya uhuru na uchumi kwa wananchi wote bila kujali nafasi zetu katika jamii," amesema Chimsinga.

Mwaka 2018, Chilima alishangaza Malawi alipomshutumu bosi wake, rais wa wakati huo, Mutharika, kwa ufisadi. Hii iliimarisha sura yake kama mpiganaji wa vita dhidi ya ufisadi.

Msimamo na mtazamo wake wa uongozi uliimarishwa zaidi alipoamua kushiriki maandamano ya kupinga udanganyifu katika uchaguzi, hata baada ya kuahidiwa uongozi wa nchi.

Chilima alikuwa Mkatoliki mcha Mungu na baba wa watoto wawili. Kifo chake kinaacha pengo katika familia yake, chama chake - ambapo hakuna mrithi wa wazi - na nchi kwa ujumla.

"Alikuwa rais bora ambaye Malawi haitawahi kuwa nayo," amesema Khumbo Soko, ambaye ni wakili wa Chilima wakati akihojiwa na The Continent.

*Makala haya ya uchambuzi, yamechapishwa kwa mara ya kwanza na The Continent, gazeti linalosambazwa kwa njia ya WhatsApp na kuchachapishwa kwa lugha ya Kiingereza. Unaweza kupata nakala yake bure, kila wiki kwa kujitandikisha kupitia namba hii: +27738056068*

## Afrika Kusini

### Vyama vikongwe Afrika vijitafakari

Na Andrew MMBONGO,  
Mbeya

**N**INA ANGALIZO kwa chama tawala nchini Afrika Kusini, ANC kinachoongzwa na Rais Cyril Ramaphosa kwa kushindwa kuunda serikali peke yake, baada ya kukusanya asilimia arobaini ya matokeo ya kura zote zilizopiga katika uchaguzi mkuu nchini humo.

Angalizo langu linalenga zaidi kueleza nini tafsiri ya kilichotokea huko Afrika Kusini baada ya chama kikongwe cha ANC, kushindwa chini ya asilimia 17 ikilinganishwa na ushindi wake katika uchaguzi uliopita.

Mkwamo wa ANC (African National Congress) katika kuunda serikali nchini Afrika Kusini una tafsiri muhimu ya kisiasa na kidemokrasia katika Bara la Afrika. Huu ni uchambuzi wa maana yake:-

**Mosi**, kupungua kwa umashuhuri wa vyama vya ukombozi; Mkwamo huu unaonyesha kupungua kwa umaarufu wa vyama hivyo ambavyo vimekuwa madarakani kwa muda mrefu baada ya uhuru.

Hii inaashiria kwamba wananchi wanatafuta mbadala na kwamba hawaridhiki tena na utendaji wa vyama hivi.

**Pili**, kuimarika kwa demokrasia; hali hii inaashiria kuimarika kwa demokrasia, ambapo vyama vya siasa vinaweza kupoteza umaarufu kutokana na utendaji mbovu na viongozi wake, hivyo kulazimika kushindana kwa uwazi zaidi ili kupata ridhaa ya wananchi. Ushindani huu unaimarisha uwajibikaji na uwazi katika utawala.

**Tatu**, uchochezi wa mageuzi ya kisiasa; mkwamo huu unaweza kuwa kichocheo cha mageuzi ya kisiasa ndani ya ANC na katika mfumo wa kisiasa wa Afrika Kusini kwa ujumla.

Vyama vinapokuwa na changamoto ya kudumisha uungwaji mkuu, vinaweza kulazimika kuboresha sera na utendaji wao.



*Cyril Ramaphosa - Rais wa Afrika Kusini*

**Nne**, uhamasishaji wa vyama vipya na sauti mbadala; hali hii inaonyesha nafasi kubwa kwa vyama vipya na sauti mbadala kushika nafasi katika siasa za kitaifa, inaweza kuhamasisha kuundwa kwa vyama vipya na kuongeza ushiriki wa wananchi katika siasa.

**Tano**, kutokuwepo kwa uhuru wa kudumu wa kisiasa; mkwamo huu unaonyesha kwamba hakuna chama chochote kilicho na uhakika wa kuendelea kushika madaraka kwa muda mrefu bila kujali utendaji wake.

Hii inawasilisha somo muhimu kwa vyama vingine barani Afrika, kwamba vinahitaji kuendelea kujenga uungwaji mkuu wa wananchi kupitia utendaji bora, haki na usawa.

**Sita**, uwezesaji wa mashirika ya kiraia na vyombo vya habari; hali hii inatoa nafasi kwa mashirika ya kiraia na vyombo vya habari kuchukua nafasi muhimu katika kusimamia na kuhimiza uwajibikaji wa serikali.

Wananchi wanapooona vyombo hivi vikifanya kazi zao vizuri, imani yao katika mfumo wa demokrasia inaimarika.

Kwa ujumla, mkwamo wa ANC katika kuunda serikali una athari kubwa kwa siasa na demokrasia Afrika, huku ukitoa somo la uwajibikaji na umuhimu wa kuboresha utendaji ili kupata ridhaa ya wananchi.

## Championi wa umeme – jua apaisha Tanzania

Na Mwandishi WETU

**M**HAMASISHAJI mkubwa wa matumizi ya umeme unaotumia nguvu ya jua kutoka Tanzania, Sisty Basil, amekuwa mshindi wa kwanza kupata nafasi ya kuhudhuria mafunzo ya vitendo kwa miezi sita nchini Marekani.

Mafunzo hayo yanayohusisha elimu zaidi ya kubuni mifumo na kusambaza nguvu ya umeme wa jua, ameyapata kutoka vituo kadhaa vikubwa vya kuzalisha nishati hiyo ya mwanga wa jua nchini Marekani, ikiwa ni ufadhili wa Taasisi ya Mott, iliyoko Michigan.

Kupitia Mfuko wa Mafunzo wa Sandra N. Smithey, chini ya Mott, Sisty ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya E-LICO Foundation, iliyoko

Dar es Salaam, ametembelea vituo vikubwa vya kusambaza nishati ya jua kwenye miradi kabambe na matumizi ya nyumbani katika maeneo kadhaa ndani ya miji ya Minnesota, Georgia, Indiana na alihudhuria mkutano maalum kuhusu mchango wa nishati ya jua katika kilimo ulioandaliwa na Benki ya Dunia jijini Washington, D.C., mapema mwezi huu – Juni, 2024.

Taasisi ya Mott katika mawasiliano yake kwa Pambazuko, imesema kuwa elimu aliyopata Sisty akiwa Marekani, itasaidia zaidi ujuzi kwa watu wengine ambao wanafanya kazi ya kuzalisha na kusambaza nishati inayotumia mwanga wa jua.

Akizungumza na Pambazuko juzi, baada ya kurejea Dar es Salaam, Sisty alisema mafunzo hayo yamefungua zaidi uelewa wake katika masuala ya nishati ya umeme na kwamba sasa yuko tayari kutumika zaidi “kuongeza kani ya umeme-jua kwa watu binafsi, taasisi, na

hata viwanda.”

Sisty amesema sehemu kubwa ya mafunzo ya vitendo aliyopata Marekani, yako katika mawanda ya matumizi ya nishati ya jua kwenye kilimo.

“Kilimo chetu kinaweza kuwa na tija zaidi, ikiwa nishati ya umeme wa jua itatumika kupeleka maji katika mashamba,” amesema Sisty.

Pambazuko linazo taarifa kuwa



*Sisty Basil, akiwa ofisi za makao makuu ya Mott*

zaidi ya watu milioni 750 katika Afrika, hawana umeme wa uhakika, huku asilimia 80 ya watu hao – karibu watu milioni 600, wakiwa wanaishi maeneo chini ya Sahara.

Taasisi ya E-LICO, anayoongoza Sisty, imekuwa “ikipambana na kuhamasisha” matumizi sahihi ya nishati ya jua, huku ikihimzia kuungwa mkono na mashrika, serikali na hata sekta binafsi, ili kuhakikisha Watanzania wanatumia zaidi nishati ya jua katika shughuli zao ili kupunguza madhara ya kutumia nguvu zingine za kuzalisha umeme ambazo ni aghali ama zinaharibu mazingira.

E-LICO, ikiwa imeanzishwa tangu mwaka 2018, imekuwa ikihusika zaidi kufundisha wananchi, hasa wa wakulima, kutumia nishati ya umeme wa jua katika shughuli zao na hata matumizi ya nyumbani.

Moja ya mafanikio makubwa ya Taasisi ya E-LICO, ni kuweza kuthibitika kupunguza uharibifu wa mazingira na , kupunguza madhara ya hewa ukaa.

## Habari

## Deni la Taifa mjadala mzito

Na Mwandishi WETU

**K**UONGEZEKA kwa deni la taifa kwa asilimia 19.1 ndani ya kipindi cha mwaka mmoja, kumeibua mjadala, hasa kwenye mitandao ya kijamii, huku wachumi wakionya matumizi makubwa ya serikali kwenye maeneo yasiyo ya ulazima mkubwa kama vile kununua magari ya thamani kubwa.

Wataalamu hao wa uchumi wametoa maoni yao ikiwa ni siku chache tu baada ya Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba kuwasilisha bungeni Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Mwenendo wa deni hilo la taifa unaonyesha kuwa Machi, 2024 lilikuwa Shilingi trilioni 91.7 ikilinganishwa na Shilingi trilioni 77 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Hili ni ongezeko la asilimia 19.1.

Kwa mujibu wa Waziri Nchemba, katika kiasi hicho cha deni la taifa, Shilingi trilioni 60.9 ni deni la nje huku lile la ndani likiwa ni shilingi trilioni 30.7.

Mchumi Mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dkt. Bravious Kahyoza, amesema sababu zinazotolewa na serikali kuhusu ukopaji huo hazina mashiko kwa sababu zimekaa kisiasa.

Akifafanua amesema sababu kubwa ya deni kukua ni kushuka kwa uzalishaji wa kutosha kwenye uchumi katika bidhaa zinazochakatwa, pia amesema taifa limejiingiza katika uwekezaji mkubwa katika miradi ya maendeleo ambao unaozidi uwezo wa pato la taifa.

Amesema kuwekeza katika miradi hiyo si jambo baya lakini ubaya ni kufanya uwekezaji ambao unzidi uwezo wa uchumi wako kuhimili kiasi cha kulazimika kukopa.

Mbaya zaidi, malighafi na bidhaa nyingi zimmazotumika katika utekelezaji wa miradi hiyo hazizalishwi nchini hivyo kufanya kiasi kikubwa cha fedha zilizokopwa kupeleka nje ya nchi.

Anafanua kuwa endapo fedha nyingi zingesalia nchi zingetumika katika



Dkt. Kahyoza

kukuza uzalishaji na hivyo kipato cha wananchi na pato la serikali kupiyya kodi.

“Mfano katika miradi hii mikubwa bidhaa zinazotumika hazizalishwi ndani ya nchi yetu, bali zinaagizwa kutoka nje sasa hapa athari zake ni makubwa ndio maana deni linaongezeka,” amesema.

Mchumi huyo alitaja sababu nyingine ya deni la taifa kuendelea kuongezeka kuwa ni matumizi makubwa ya serikali kuliko uwezo wake hasa kwenye kununua na kuhudumia magari.

“Mwaka jana Mwigulu alionya kuwa angechukua hatua kuhusu matumizi hayo kwa sababu ilikuwa imetumika Shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kununua magari na kuyahudumia, lakini hakuchukua hatua yoyote na gharama hiyo imepanda tena hadi kufikia shilingi bilioni 800.4,” ameongeza msomi huyo.

Amesema serikali ingebana matumizi hayo na mengine kila mwaka, ingekuwa inaokoa Shilingi trilioni 1.2.

Kwa upande wake, mwanasheria na mwanaharakati, Dkt. Hellen Kijo Bisimba amesema sababu zilizotolewa na serikali kuhusu deni la taifa kuongezeka, hazina tija kwa sababu hakuna matokeo ya

## Deni la Taifa mjadala mzito

**Inatoka Uk. 22**

maendeleo yanayoonekana.

“Serikali inakopakopa tu hata hayo maendeleo hatuyaoni badala yake maisha yanazidi kuwa magumu na kila kitu kinasuasua tu, halafu wanatumbia deni hilo ni deni letu kwa sababu sisi wananchi ndio walipaji...”

“... Nilitegemea bunge ambalo ndilo msemaji mkuu kwa niaba yetu wananchi, litusemee, lakini inaonekana nalo limeshindwa kushauri serikali. Angalau kidogo spika aliyepita (Job Ndugai) aliwahi kusema kwamba tusikope bila kujua tunarudishaje na unapochelewa riba zinazidi kuongezeka,” ameongeza Dkt. Bisimba.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. George Kahangwa alisema Serikali ina wajibu wa kuwathibitisha Watanzania kwamba maelezo wanayoyotoa ni ya uhakika.

Amesema kuna haja pia Serikali ikaweka wazi mpango wake wa kulipa madeni hayo ili kulipunguzia taifa wasiwasi.

Kuhusu nini kifanyike kuhakikisha kuwa deni halikui ili kupunguza mzigo kwa wananchi kulipa madeni hayo, Dkt. Kahangwa amesema ipo haja ya kuwa na nidhamu ya hali ya juu ya katika kukopa.

“Tuepuke kukopa holela, tusikope tu eti kwa sababu wakopeshaji wapo. Tunahitaji pia nidhamu katika matumizi ya fedha zitokanazo na mikopo hiyo pamoja na fedha nyinginezo...”

“... Fedha zilizokopwa sharti zitumike tu katika shughuli zinazotuzalishia faida na kukuza uchumi...”

“... Hali tukijua tunadaiwa sana, Watanzania tuna wajibu wa kuongeza uzalishaji maradufu katika sekta zote za uchumi. Tunapaswa kuwatumia wataalamu wetu wa ndani, watutengenezee mifumo ya uzalishaji

kwenye kila eneo ili kujikwama kutoka hapa tulipo,” amesisitiza Dkt. Kahangwa.

Wakati Dkt. Nchemba akiwasilisha bajeti hiyo alisema tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Desemba 2023, imeonyesha kuwa deni ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

Alisema katika tathmini hiyo, viashiria vinaonesha kuwa kwa mwaka 2023/24, thamani ya sasa ya deni la serikali ni asilimia 35.6 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55.

Alieleza kuwa thamani ya sasa ya deni la nje ni asilimia 19 ya Pato la Taifa, ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40 na thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 113.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180.

### Kwa nini deni linaongezeka

Dkt. Nchemba alisema ongezeko la deni la taifa limechangwa na sababu kadhaa za msingi za maendeleo ikiwa ni pamoja na kupokea fedha kutoka

mikopo ya zamani na mipya ambapo fedha hizo zimeelekezwa kwenye miradi ya maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli ya kisasa, viwanja vya ndege na miradi ya umeme, elimu na afya.

Alisema kwa kipindi cha kuanzia Aprili 1, 2021 hadi Machi, 2024, Serikali ilipokea jumla ya Shilingi trilioni 17.2.

Waziri huyo wa fedha alisema sababu nyingine ya kukua kwa deni ni kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani.

Akifafanua alisema kuwa na kuanzia Machi 13, 2021 hadi Machi 31, 2024, thamani ya Shilingi dhidi ya dola moja ilipungua kutoka Shilingi 2,309.96 hadi 2,569.66, sawa na kupungua kwa asilimia 11.24.



**Dkt. Bisimba**

# NENDA SALAMA CHILIMA...



Makamu wa Rais wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango amemwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika mazishi ya kitaifa ya aliyekuwa Makamu wa Rais wa Malawi, Dkt. Saulos Klaus Chilima. Ibada ya mazishi hayo ilifanyika katika Uwanja wa Taifa wa Bingu uliopo Jiji la Lilongwe, Malawi. (Picha kutoka x.com/VPTanzania).

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.